

Bibilia ya watoto

Inaleta

Mungu
Ajaribu
Pendo la
Ibrahimu



Kimeandikwa na: Edward Hughes
Kimeorodheshwa na: Byron Unger; Lazarus
Alastair P.

Imerekebishwa na: M. Maillot; Tammy S.

Kimetafsiriwa na: Grace Chepkoech

Kimedhibitishwa na: Bible for Children

www.M1914.org

BFC

PO Box 3

Winnipeg, MB R3C 2G1

Canada

©2020 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.






Usiku mmoja Mungu
alimwamuru
Ibrahimu. Ilikuwa
jaribu kuona kama
Ibrahimu alimpenda
mwanawe Isaka
* kumliko Mungu.




"Mchukue mwanawe Isaka
na ukamtoe kama sadaka ya
kuteketezwa," Mungu aliamuru.

Kumtoa Isaka?
Kumtoa mwana wake
kama sadaka? Hii
ilikuwa ngumu kwa
Ibrahimu. Yeye
alimpenda mwanawe
sana.





Lakini Ibrahimu alikuwa
amejifunza kumwuamini
Mungu hata kama hakuwa
anaelewa. Asubuhi na mapema
aliondoka kuelekea mlima wa

sadaka pamoja na Isaka
na vijana
wawili.



Kabla kuondoka,
Ibrahimu alichanja
kuni ya moto ya
kuteketeza sadaka.
Ibrahimu alipanga
kumtii Mungu.





Baada ya siku tatu walikaribia mlima ule. "Kaeni hapa," Ibrahimu akawaambia vijana wale wawili, vijakazi wake. "Tutaenda na kuabudu alafu tutarudi."

Isaka alibeba kuni; Ibrahimu akabeba moto - na kisu.




"Yuko wapi mwana kondoo wa kutoa sadaka?" Isaka akauliza. "Mungu atatupa mwana kondoo," Ibrahimu akamjibu.




Wakaja hadi mahali Mungu alikuwa amechagua. Pale. Ibrahimu akajenga madhabahu na akapanga kuni ya kuteketeza sadaka mbele ya Mungu. Ibrahimu alikuwa amejenga madhabahu mingi. Lakini hii ilikuwa ngumu zaidi kuliko zote.





Ibrahimu
alimfunga Isaka
kwa kamba na
akamwekelea mwana
wake mpendwa juu ya
madhabahu. Je, Ibrahimu
angemtii Mungu na kumtoa sadaka
Isaka, mwana wake wa pekee?
Ndio! Kisu ilitoa mwangaza
Ibrahimu alipokuwa akiinua
juu. Labda moyo wake
ulikuwa unavunjika, lakini
Ibrahimu alijua ni lazima
amtii Mungu.






"WACHA!"
malaika wa
Mungu
akanena.
"Sasa ninajua
kuwa
unamwogopa
Mungu.
Hukunizuilia
mwanao wa
pekee."



Alipomwona kondoo mume kichakani, Ibrahimu alimfungua Isaka na akimtoa kondoo yule kama sadaka wa kuteketezwa. Labda Isaka alifikiria, "Mungu ametupa kondoo, kama vile baba alisema."



Wakati baba na mwanawe waliendelea kuabudu, malaika wa Mungu alinena na Ibrahimu. "Kupitia watoto wako, mataifa yote yatabarikiwa kwasababu umetii." Siku moja, Yesu angezaliwa kupitia kizazi cha Ibrahimu.



Ibrahimu na Isaka wakarudi nyumbani. Baada ya muda mrefu kupita, huzuni ukaja. Sara akafa. Ibrahimu alipoteza mkewe na Isaka alimpoteza mamaye.



Baada ya mazishi,
Ibrahimu alimtuma mk-
ubwa wa watumishi wake
amtafutie Isaka mke. Mtumishi
alienda walipokuwa wakiishi zamani kumta-
futa mke kati ya jamaa wa
Ibrahimu.



Mtumishi alimwomba Mungu ishara. "Binti yule ambaye atajitolea kuwanywasha ngamia wangu maji ndiye atakuwa mke wa Isaka." Punde Rebeka akajitolea kuwapa ngamia wake maji. Rebeka alikuwa mmoja wa jamaa wa Ibrahimu. Mtumishi yule akajua kuwa

Mungu alikuwa amejibu ombi lake.



Rebeka aliwacha familia yake kuenda kumwoa Isaka.
Alimfariji baaada ya kifo cha mama yake. Isaka
alimpenda sana!



Mungu Ajaribu Pendo la Ibrahimu

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Mwanzo 22-24


"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."

Zaburi 119:130





5



60



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

